MALEZI YANAYOREFUSHA MIZIZI YA IMANI KWA MTOTO

Kumbukumbu 6:6-7



Mch Denis & Devis Julius

MALEZI YANAYOREFUSHA MIZIZI YA IMANI KWA MTOTO

Andiko kuu: Kumbukumbu la Torati 6:6–7

Shalom! Nakusalimu katika jina kuu la Bwana wetu Yesu Kristo, karibu tujifunze Hekima za Mungu katika maandiko kuhusu malezi bora ya watoto,

Tunaweza kujiuliza swali moja muhimu: Kwa nini watoto wengi wa siku hizi, ijapokuwa wanafundishwa Neno la Mungu, wanapelekwa makanisani na kushiriki mafundisho ya kiroho, lakini bado hawana msingi imara wa kumjua Mungu katika maisha yao?

Kwa nini wengine wanapokuwa chini ya uangalizi wa wazazi wao wanaonekana kuwa na mwenendo mzuri, lakini wanapokuwa mbali na wazazi wao wanashindwa kusimama katika imani?

Hili ni swali ambalo kila mzazi/ mlezi Mkristo anapaswa kujiuliza.

Ipo kanuni muhimu ya malezi ambayo imesahaulika tunayoisoma katika

Kumbukumbu la Torati 6:6–7.

Inasema;

> "Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo."

Kabla hatujaangalia kwa undani hatua hizo,

Mungu anaanza kwa kusema: "Na maneno haya ... yatakuwa katika moyo wako."

Hili ni jambo la muhimu sana. Mungu hakuanza kwa kusema wafundishe watoto wako, bali alianza kwa kuelekeza kwamba Neno lake liwe kwanza katika moyo wa mzazi.

Hii inatufundisha kwamba malezi ya kiroho ya mtoto huanza na maisha ya kiroho ya mzazi.

Huwezi kumfundisha mtoto kumpenda Mungu ikiwa wewe mwenyewe huna nafasi ya Neno la Mungu katika maisha yako. Huwezi kumfundisha mtoto kuwa mtu wa maombi ikiwa yeye haoni mfano wa maisha ya maombi nyumbani.

Kwa hiyo, kabla mtoto haj

Kwa hiyo, kabla mtoto hajajifunza kutoka katika maneno yetu, anajifunza pia kupitia mwenendo wetu.

Ndiyo maana tunapaswa kuwa watu wa Neno, watu wa maombi na watu wanaoishi kile tunachowafundisha watoto wetu.

Baada ya kuweka msingi huo, sasa tuangalie maeneo manne ambayo Mungu ameyaweka katika andiko hili.

1. UNAPOKETI NYUMBANI KWAKO

Biblia inasema: "Na kuyanena uketipo katika nyumba yako."

Maana yake ni kwamba unapoketi pamoja na watoto wako nyumbani, wakati wa mazungumzo, wakati wa chakula au mapumziko, tumia nafasi hiyo kuwafundisha mambo ya Mungu.

Mara nyingi wazazi tunapokuwa na watoto nyumbani, mazungumzo yetu yanahusu shule, chakula, kazi, mavazi na mahitaji mengine ya

maisha. Haya yote ni muhimu, lakini tusisahau pia mazungumzo yanayohusu ukuaji wao wa kiroho.

Kwa mfano, unaweza kumwuliza mtoto:

Leo umejifunza nini kuhusu Mungu?

Kuna jambo gani lililokushawishi kufanya jambo baya leo, kama vile kukasirika, kupayuka?

Ungefanya nini kama rafiki yako angekushawishi udanganye?

Unafikiri kwa nini tunapaswa kuwasamehe watu wanaotukosea?

Maswali haya yanamsaidia mtoto kufikiri kwa misingi ya Neno la Mungu badala ya kujifunza tu kukariri mistari ya Biblia.

Pia, tengeneza utaratibu wa kuwa na ibada fupi ya familia. Mnaweza kusoma andiko moja, kueleza ujumbe wake, kuimba wimbo mmoja na kuomba pamoja.

2. UNAPOTEMBEA NJIANI

Biblia inasema: "Na utembeapo njiani."

Hii inatufundisha kwamba malezi ya kiroho hayapaswi kufungwa ndani ya nyumba au kwenye muda maalumu wa ibada. Hata wakati wa kutembea na mtoto, kuna nafasi ya kumfundisha njia ya haki.

Kwa mfano, unapokuwa unatembea naye na mkakutana na mtu mwenye uhitaji, unaweza kumfundisha umuhimu wa kusaidia wengine.

Mnapoona mtu akifanya jambo lisilo la haki, unaweza kumweleza kwa nini Mkristo anapaswa kusimama katika kweli hata kama watu wengine wanafanya tofauti.

Unapokuwa naye safarini, unaweza kumweleza kuhusu uumbaji wa Mungu, wema wake na jinsi tunavyopaswa kumshukuru kwa mambo mbalimbali tunayoyaona.

Mazingira ya kawaida ya maisha yanaweza kuwa darasa la kumfundisha mtoto kumjua Mungu.

Usifikiri kwamba ili mtoto ajifunze Biblia ni lazima ukae naye na kufungua kitabu cha Biblia pekee. Unaweza kutumia tukio lolote la kawaida kumsaidia kuelewa kanuni ya kiroho.

Kwa hiyo, tunapokuwa na watoto wetu, tuwe na utayari wa kutumia mazingira yanayotuzunguka kuwafundisha njia ya haki.

3. UNAPOLALA

Biblia inasema: "Na ulalapo."

Hii inatuonyesha kwamba hata wakati wa kupumzika, mtoto anapaswa kuendelea kujengwa katika mambo ya Mungu.

Kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na muda wa kumfundisha mtoto kabla hajalala. Huu ni wakati mzuri kwa sababu shughuli nyingi za siku huwa zimekwisha, na mzazi anaweza kupata nafasi ya kuzungumza naye kwa utulivu.

Kwa mfano, kabla mtoto hajalala, unaweza kufanya mambo yafuatayo:

Kusoma naye kifungu kifupi cha Biblia.

Kumweleza maana ya andiko mlilosoma.

Kumwuliza amejifunza nini katika siku hiyo.

Kumsaidia kutambua makosa aliyoyafanya na kumfundisha namna ya kuyarekebisha.

Kuomba pamoja naye kabla ya kulala.

Kwa mfano, unaweza kumsomea Waefeso 4:32 kuhusu kuwa wafadhili na kusameheana. Kisha umweleze umuhimu wa kutokulala akiwa amebeba chuki dhidi ya ndugu yake au mtu aliyemkosea.

Lakini pia, kuna jambo lingine muhimu. Mfundishe mtoto kuomba mwenyewe, si kusubiri kila wakati mzazi amwombee. Mpe nafasi ya kumshukuru Mungu, kuomba msaada na kueleza mahitaji yake kwa Mungu kwa maneno yake mwenyewe.

Hii itamsaidia kujenga maisha binafsi ya maombi.

Lengo si mtoto kuzoea kuomba kwa sababu mzazi amemwambia aombe, bali kumsaidia kuelewa kwa nini anahitaji kuwa na uhusiano wake binafsi na Mungu.

4. UONDOKAPO (UNAPOAMKA)

Biblia inasema: "Na uondokapo."

Hapa tunaona kwamba mafundisho ya Mungu yanapaswa kuendelea hata tunapoanza shughuli za siku.

Mtoto anapoamka asubuhi, usimfundishe tu kuamka, kuoga, kuvaa na kwenda shule. Mfundishe pia namna ya kuanza siku yake akiwa na Mungu.

Kwa mfano, unaweza kumfundisha:

Kumshukuru Mungu kwa kumlinda usiku.

Kuomba kabla ya kuanza shughuli zake.

Kuwa mwaminifu katika mambo madogo.

Kuepuka marafiki wanaomshawishi kufanya mabaya.

Kumheshimu Mungu hata akiwa mbali na wazazi wake.

Unaweza pia kumfundisha mstari mmoja wa Biblia ambao atautafakari katika siku hiyo.

Kwa mfano, Mithali 3:5 inatufundisha kumtumaini Bwana kwa moyo wetu wote.

Mfundishe kwamba anapokuwa shuleni, anapocheza na wenzake au anapokutana na majaribu, anapaswa kukumbuka kwamba yeye ni

mtoto anayepaswa kumheshimu Mungu katika mwenendo wake.

Kumbuka, mtoto anapokuwa shuleni, mzazi hayupo kila wakati kumwambia afanye nini. Ndiyo maana tunapaswa kumjenga awe na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi hata pasipo uwepo wetu.

Hii ndiyo sababu mafundisho ya asubuhi yana umuhimu mkubwa: yanamsaidia mtoto kuanza siku akiwa na mwelekeo wa kiroho.

5. KANUNI NYINGINE MUHIMU: USIMFUNDISHE KWA MANENO PEKEE, MFUNDISHE KWA MFANO

Mbali na maeneo hayo manne, kuna jambo lingine ambalo wazazi tunapaswa kulizingatia.

Mtoto hujifunza mambo mengi kwa kuangalia mwenendo wa wazazi wake.

Ikiwa unamfundisha mtoto kutosema uongo, lakini yeye anakuona ukidanganya, utakuwa unampa mafundisho mawili yanayopingana.

Ikiwa unamfundisha kusamehe, lakini ndani ya nyumba anaona chuki, ugomvi na

kutokusameheana, itakuwa vigumu kwake kuelewa vizuri somo hilo.

Ndiyo maana Waefeso 6:4 inawaagiza akina baba wasiwachokoze watoto wao, bali wawalee katika adabu na maonyo ya Bwana.

Hii inamaanisha kwamba malezi ya kiroho yanahitaji hekima, upendo na nidhamu.

Usitumie Biblia kama chombo cha kumtisha mtoto kila wakati. Msaidie kuelewa upendo wa Mungu, utakatifu wake na matokeo ya matendo yake.

Mtoto anapokosea, mrekebishe. Anapofanya vizuri, mtie moyo. Anapouliza swali, msikilize. Anaposhindwa, msaidie kuinuka, lakini pale anapokosea kwa ujinga mwadhibu huku akijua kosa lake.

6. KWA NINI MAFUNDISHO HAYA NI MUHIMU SANA?

Kuna sababu kubwa inayotufanya tusisitize malezi haya ya kila siku.

Watoto wetu watakuja kufika katika mazingira ambayo hatutakuwa karibu nao.

Wengine wataenda shule za bweni, wengine watakwenda vyuoni, wengine wataanza kazi na wengine wataishi katika maeneo tofauti na wazazi wao.

Wakati huo, hatutakuwa na uwezo wa kuwaambia kila siku waombe, wasome Biblia, waepuke marafiki wabaya au wafanye maamuzi sahihi.

Ndiyo maana tunapaswa kuwaandaa mapema.

Katika 2 Timotheo 3:15, tunaona mfano wa Timotheo ambaye tangu utoto wake aliyajua Maandiko Matakatifu.

Hili linatufundisha kwamba mtoto anaweza kuanza kujengwa katika maarifa ya Maandiko tangu akiwa mdogo.

Usisubiri mtoto akue ndipo uanze kumfundisha kuomba. Usisubiri aingie katika changamoto za ujana ndipo uanze kumfundisha namna ya kushinda majaribu. Usisubiri aende mbali na wewe ndipo uanze kumfundisha namna ya kuwa na muda binafsi na Mungu.

Mfundishe sasa, wakati bado una nafasi ya kuwa karibu naye.

HITIMISHO

Kwa hiyo, tunapojifunza Kumbukumbu la Torati 6:6–7, tunaona kwamba Mungu hakutaka malezi ya kiroho ya mtoto yaishie katika kumpeleka kanisani Jumapili au kumfundisha kwa muda mfupi jioni.

Anataka Neno lake liwe sehemu ya maisha ya kila siku ya mtoto.

Kuna maeneo manne muhimu tunayopaswa kuyazingatia:

Unapoketi: Tumia muda wa mazungumzo ya nyumbani kumfundisha mtoto njia ya haki.

Unapotembea: Tumia mazingira na matukio ya kawaida kumjenga kiroho.

Unapolala: Msaidie kuwa na muda wa Neno la Mungu, kutafakari na maombi.

Unapoamka: Mfundishe kuanza siku yake kwa kumtegemea Mungu na kuishi katika kweli.

Na zaidi ya yote, hakikisha kwamba unakuwa mfano wa yale unayomfundisha.

Wazazi, tusiridhike kwa watoto wetu kujua majina ya vitabu vya Biblia, kujua nyimbo za kanisani au kuhudhuria Sunday School. Tujitahidi kuwasaidia wajenge uhusiano binafsi na Mungu.

Lengo letu si kuwafanya watoto wetu wawe Wakristo wazuri pale tunapowaona, bali kuwajenga wawe watu wanaomcha Mungu hata pale ambapo hatupo pamoja nao.

Siku moja watatembea peke yao, watafanya maamuzi yao wenyewe na watakutana na majaribu ambayo hatutaweza kuyashughulikia kwa niaba yao. Lakini ikiwa tutawajenga vizuri katika Neno la Mungu, watakuwa na msingi wa kiroho utakaowasaidia kusimama.

Mungu atusaidie tusipuuze wajibu huu mkubwa ambao ametukabidhi kama wazazi.

Mungu awabariki wazazi wote wanaojitahidi kuwalea watoto wao katika njia ya haki. Amina!

MASWALI YA KUTAFAKARI KWA KILA MZAZI

Jiulize!

Je, watoto wangu wanajifunza kuhusu Mungu nyumbani au wanategemea mafundisho wanayopata kanisani pekee?

Je, nina muda maalumu wa kusoma Biblia na kuomba pamoja na watoto wangu kila siku?

Je, mwenendo wangu wa kila siku unafundisha kile ninachowaambia watoto wangu?

Je, nikimwacha mtoto wangu mbali nami kwa muda mrefu, atakuwa na msingi wa kiroho wa kumsaidia kusimama katika imani yake?

Bwana akubariki.

Shalom.

Kwa mawasiliano

Kanisa La Nuru ya Upendo

Mch. Denis & Devis J. Magembe

Tel: +255693036618 / +255789001312

E-mail: info\@wingulamashahidi.org